Somo la 37　富士山を見たり、おすしを食べたりしました

FUJISAN O MITARI, OSUSHI O TABETARI SHIMASHITA

寮母 Msimamizi wa bweni	旅行はどうだった？ RYOKÔ　WA　DÔ　DATTA?	Safari yako ilikuwaje?
アンナ Anna	富士山を見たり、おすしを食べたりしました。楽しかったです。 FUJISAN　O　MITARI,　OSUSHI　O　TABETARI　SHIMASHITA. TANOSHIKATTA　DESU.	Niliona mlima Fuji, nikala sushi, na kadhalika. Nilifurahia.
寮母 Msimamizi wa bweni	それはよかったわね。 SORE　WA　YOKATTA　WA　NE.	Ilikuwa nzuri.

Vidokezo vya sarufi

① Kitenzi cha umbo la TA + RI, Kitenzi cha umbo la TA + RI SHIMASU

◈ Unapotoa mifano miwili ama mitatu miongoni mwa vitendo kadhaa, unatumia vitenzi vya umbo la TA na kuongeza RI baada ya kila kitenzi cha umbo la TA kwa mfuatano. Mwishoni, unamalizia sentensi kwa kutumia SHIMASU (kufanya) au SHIMASHITA (nilifanya).

k.m.)　FUJISAN O MITA　(Niliona mlima Fuji)　　OSUSHI O TABETA (Nilikula sushi)

FUJISAN O MITARI, OSUSHI O TABETARI SHIMASHITA.

(Niliona mlima Fuji, nikala sushi, na kadhalika.)

② _ WA DÔ DATTA?　(_ ilikuwaje ?)

◈ DÔ inamaanisha "vipi/namna gani." DATTA ni kauli ya kawaida ya DESHITA, ambayo humalizia sentensi kwa hali ya wakati uliopita.

k.m.) SHIKEN WA DÔ DATTA? (Mtihani ulikuwaje?)

Tanakali Sauti

Unasema hivi unapokuwa umechoka na kuhisi kuwa dhaifu.

Unasema hivi unapokuwa umechoka kabisa, na kuhisi kana kwamba umeishiwa nguvu.

Imetayarishwa na NHK WORLD © ver. April 2015